
# ARDHI NI UHAI

HAKIARDHI
LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

ISSN NO. 0856-9495 | TOLEO LA 14 | AGOSTI - DESEMBA 2015


## NAFASI YA SHERIA ZA ARDHI KATIKA KULINDA HAKI ZA WANAWAKE

*Na: Beatha Fabian*




*Cheti cha hakimiliki ya kimila ni mojawapo ya haki ya kisheria inayotolewa na Sheria ya Ardhi ya Kijiji katika kulinda haki za ardhi kwa wanawake*

Katiba ya Tanzania inampatia kila mtu haki ya kumiliki mali. Haki hiyo pia inalindwa na Sheria ya Ardhi namba.4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba. 5 za mwaka 1999. Kulingana na Sheria hizi, mtu au watu wanaoweza kuomba haki ya umiliki wa ardhi ni pamoja na mwanamke au mwanaume mtanzania mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea. Hivyo wanawake wanaweza kupata ardhi kwa njia ya kununua, kupewa zawadi, kugawiwa na serikali au kugawiwa kurithi mila, desturi na taratibu za sheria husika. Wakati mila na desturi za kitanzania zimekuwa zikiwanyima wanawake haki ya kupata, kutumia, kumiliki na kudhibiti ardhi moja kwa moja, sheria zote mbili zimetatua suala hili.

Sheria za ardhi zimeondoa desturi za kibaguzi ambazo ziliathiri haki za wanawake kumiliki ardhi na kutambua usawa wa wanawake na wanaume katika kumiliki ardhi. Wanawake wana haki katika kumiliki ardhi kimila, haki ambayo hapo awali ilikuwa haipo na kama ilikuwepo basi ni katika baadhi ya mila na desturi nzuri japokuwa ni chache.

Wanawake wanapaswa watambue kuwa umiliki wa kisheria na wa kimila una hadhi sawa na wa mwanaume na pia kuna utaratibu wa kisheria mara baada ya kupata ardhi ili kuboresha umiliki wake ni hati maalum kulingana na eneo la ardhi au nyumba ilipo (mjini au kijijini)


*Inaendelea uk. 3* ››


## MSAADA WA KISHERIA UNAIMARISHA ULINZI WA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE.

*Na. Nakamo Tenende*

HAKIARDHI imekuwa ikifanya tafiti katika wilaya mbalimbali nchini kuanzia ilipoanzishwa mwaka 1994. Baadhi ya tafiti zimebainisha kuwa wananchi wanaoishi katika ngazi za msingi hususan vijijini wakiwemo wanawake, wafugaji, waokota matunda na wachimbaji wadogo wamekosa haki zao katika ardhi kutokana na mtazamo hasi wa jamii juu ya mwanamke kumiliki ardhi, kushamiri kwa mfumo usiozingatia haki na usawa katika upatikanaji, uzalishaji na mgawanyo wa mali na rasilimali. Dosari hii inaanzia katika ngazi ya familia hadi ngazi za juu za kiutawala katika serikali kuu huku zikilindwa na baadhi ya sera na sheria. Wanawake wamekuwa ni wahanga wakubwa katika kukosekana huku kwa usawa na haki. Ndiyo maana, HAKIARDHI kwa kutambua hilo, imekuwa na kawaida ya kutoa ushauri na msaada wa kisheria kwa wananchi vijijini, mpango ambao umewezesha wanawake wengi kupata haki ya kupata, kutumia na kumiliki ardhi na rasilimali nyinginezo katika maeneo yao.

Msaada wa kisheria umetolewa katika maeneo mengi ya vijijini na pembezoni mwa miji kwa kuwatumia wanasheria wa Taasisi ya HAKIARDHI pamoja na wangalizi wa Masuala ya ardhi waliojengewa uwezo katika maeneo ambayo Taasisi imekuwa

> *"Baadhi ya tafiti zimebainisha kuwa wananchi wanaoishi katika ngazi za msingi hususan vijijini wakiwemo wanawake, wafugaji, waokota matunda na wachimbaji wadogo wamekosa haki zao katika ardhi*


*Inaendelea uk. 4* ››


YALIYOMO


- NAFASI YA SHERIA ZA ARDHI KATIKA KULINDA HAKI ZA WANAWAKE 1-3
- MSAADA WA KISHERIA UNAIMARISHA ULINZI WA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE. 1-4
- MILA POTOFU ZINA ATHIRI UMILIKI WA ARDHI KWA WANAWAKE 5
- HATIMILIKI YA KIMILA NA ULINZI WA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE 6
- ATHARI ZA MIGOGORO YA ARDHI KWA WANAWAKE 8
- NAFASI YA WANAWAKE KATIKA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI 10-11



ARDHI N/ UHAI

NAFASI YA SHERIA ZA ARDHI KATIKA KULINDA HAKI ZA WANAWAKE

**ARDHI NI UHAI** Ni jarida la Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI) ambalo hutolewa mara tatu kwa mwaka.

Kusudi kubwa ni kuwapa wadau wa Taasisi hii taarifa mbalimbali zinazohusiana na mambo ya ardhi

**Mhariri**

Yefred Myenzi

**Bodi ya Wahariri**

| | | |
|---|---|---|
| Yefred Myenzi | - | M/Kiti |
| Cathbert Tomitho | - | Mjumbe |
| Nakamo Tenende | - | Mjumbe |
| Grace Mpangala | - | Mjumbe |
| Mchapishaji | - | HAKIARDHI |
| Mchapaji | - | iPrint |
| Msanifu | - | Bakari Kacheuka |

**UJUMBE WA BODI KWA WASOMAJI**

wasomaji wa jarida hili nakaribishwa kutoa michango yenu kwa kuuliza maswali, kutoa ushauri, maoni, au kwa kuandika makala (zisizozidi kurasa tatu) kwa mhariri kupitia anuani zifuatazo:

HAKIARDHI

LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

Kitalu No.236 Block 47 Sinza Mori, Mkabala na Wanyama Hotel, S.L.P 75885, Dar es Salaam

Simu +255 22 2771360/ 0784 646752,

Nukushi: +255 22 2771362

Baruapepe: info@hakiardhi.org,

Tovuti: www.hakiardhi.org





# Mwanamke ana haki sawa ya kumilikishwa ardhi kutoka kwenye mamlaka husika

*Makala mbalimbali zimejaribu kuainisha na kuchambua haki ya mwanamke inavyojitokeza na kulindwa katika sera na sheria za ardhi*

Moja ya kanuni za msingi za sera ya taifa ya ardhi ya mwaka 1995 ambayo pia imewekewa msisitizo na sheria za ardhi za mwaka 1999, ni haki sawa kati ya mwanaume na mwanamke katika kupata, kutumia na kumiliki ardhi. Msisitizo huu ulilenga kutokomeza vitendo vya kibaguzi dhidi ya wanawake kumiliki na kunufaika na ardhi kwa misingi ya mila, desturi mitazamo hasi ya kijinsia na sababu nyingine za kitamaduni.

Katika toleo hili la 14 la jarida la Ardhi ni Uhai, makala mbalimbali zimejaribu kuainisha na kuchambua haki ya mwanamke inavyojitokeza na kulindwa katika sera na sheria za ardhi na kisha kuweka msisitizo katika utekelezaji wa vifungu vinavyobainisha haki hizo ili zisibakie kwenye vitabu vya sheria tu lakini zidhihirike katika uhalisia wa maisha ya kila siku.

> SHERIA ZIMETOA NAFASI KUBWA YA WANAWAKE KUSHIRIKI KATIKA VYOMBO VYA MAAMUZI JUU YA ARDHI KAMA VILE HALMASHAURI YA KIJIJI

Uchambuzi umeonyesha bayana kuwa mwanamke ana haki sawa ya kumilikishwa ardhi kutoka kwenye mamlaka husika bila kulazimika kupitia mgongo wa mwanaume. Hali kadhalika, sheria zimetoa nafasi kubwa ya wanawake kushiriki katika vyombo vya maamuzi juu ya ardhi kama vile Halmashauri ya kijiji ambapo robo ya wajumbe wake sharti wawe wanawake, baraza la ardhi la kijiji ambapo idadi yao haipaswi kupungua watatu katika saba na baraza la kata wasiopungua watatu kati ya wajumbe watano hadi nane. Sheria pia zimeainisha fursa nyingine za kumiliki ardhi kwa pamoja na mwenzi wake katika familia na kushirikishwa kikamilifu pale ardhi ya familia inapowekwa rehani.

Hata hivyo, licha ya fursa zote hizo, bado kuna changamoto kubwa zinazowakabili wanawake wengi kumiliki na kunufaika na ardhi katika familia zao. Baadhi yake zimeanishwa katika makala za toleo hili kuwa ni uelewa hafifu wa sheria za ardhi, mila kadamizi, kasi ndogo ya utekelezaji wa vifungu vya sheria vinavyolinda haki za wanawake na kushamiri kwa mfumo dume katika jamii nyingi za Kitanzania unaowazuia wanawake kumiliki mali sawa na wanaume.

Wito unatolewa kwa serikali, asasi za kiraia na washirika wa maendeleo kuweka mipango madhubuti itakayowezesha utekelezaji wa sheria za ardhi kikamilifu ili haki zilizoainishwa katika sheria hizo kwa wanawake ziweze kutekelezwa. Aidha, elimu kwa umma itasaidia kubomoa mfumo dume ulioota mizizi katika jamii nyingi na kuwezesha wanawake kufurahia haki ya ardhi sawa na haki ya mwanaume kwa kiwango kile kile

**Yefred Myenzi**
**MHARIRI**

» Inatoka uk. 1

# NAFASI YA SHERIA ZA ARDHI KATIKA KULINDA HAKI ZA WANAWAKE

Katika kulinda na kusimamia maslahi ya wanawake kwenye ardhi, sheria za ardhi za mwaka 1999 zimeainisha mabaraza na mahakama za utatuzi wa migogoro ya ardhi ambapo muundo wake umebainisha idadi ya wajumbe wanawake. Ukilinganisha na njia nyingine za kupata ardhi kama zilivyoainishwa hapo juu, utaratibu wa kupata ardhi kwa njia ya mirathi kwa mwanamke bado unasumbua hasa kwa makabila yanayoendeleza mila za kibaguzi. Hii ni kutokana na kukosekana kwa sheria moja ya mirathi ambayo inatumika kwa watu wote bila kujali dini, kabila wala rangi na hivyo kunasababisha wanawake kunyimwa haki yao ya kumiliki ardhi wakati waume zao wanapofariki dunia.

Kwa hali ilivo sasa, zipo aina tatu za nafasi ya mwanamke katika kumiliki ardhi kupitia mirathi. Moja, ni Sheria ya Mirathi iliyotungwa na bunge inayotumika kwa wakristo na watu wenye asili ya Ulaya, pili ni sheria ya Kiisalmu ihusuyo mirathi inayotumiwa na waislam. Hizi sheria mbili zinawapa wanawake (wajane) nafasi ya kurithi sehemu ya mali kwa mchanganuo maalum. Sheria ya tatu ni ya kimila ambayo inasema mjane hawezi kurithi nyumba wala ardhi ya marehemu mume wake. Kama mjane atataka kuegemea katika sheria ya mirathi na kuachana na sheria ya kimila, anatakiwa kuthibitisha kuwa hajaishi katika ndoa husika kwa kufuata taratibu za kimila na kijadi ili aweze kurithi. Katika mahusiano ya ndoa, sheria za ardhi zinafafanua kuhusu umiliki wa ardhi kwa pamoja na usio wa pamoja.

> “Sheria pia inaruhusu mwanandoa kumiliki ardhi binafsi

Wanandoa wanaweza kuomba umiliki wa ardhi kwa pamoja katika maslahi yanayogawanyika au yasiyogawanyika. Katika umiliki wa pamoja kwa maslahi yasiyogawanyika inatolewa kwa wanandoa moja kwa moja na ndoa hiyo inapaswa iwe halali . Ila kwa watu ambao sio wanandoa, ni sharti kwanza wapate kibali cha mahakama kupata umiliki wa aina hii katika ardhi husika. Katika umiliki wa aina yoyote yaani wa maslahi yanayogawanyika na yasiyogawanyika, ni lazima majina ya wamiliki wote yawepo kwenye hatimiliki na kila mmoja awe na nakala ya hatimiliki hiyo. Hivyo, nafasi ya mwanamke kwa maana ya maslahi yake katika umiliki wa aina hii ya ardhi inalindwa kwa kuwa hakuna mmiliki au wamiliki watakaoruhusiwa kuuza, kugawa, kuhamisha, kubadilisha umiliki au kuweka rehani ardhi pasipo kushirikisha mmiliki mwenzie na ridhaa yake kuainishwa kwa maandishi.

Sheria pia inaruhusu mwanandoa kumiliki ardhi binafsi. Katika hili ni sharti maslahi ya umiliki huu yawekwe bayana kuanzia awali kabisa pale mwanandoa mmoja wapo anapoomba umiliki wa ardhi husika. Mathalani, atapaswa kuainishwa kuwa anachukuwa hakimiliki hiyo kwa ajili yake binafsi kwa maslahi yasiyogawanyika. Kwa uzoefu wa misaada ya kisheria inayotolewa na Taasisi, jambo hili limeonekaana kusahaulika kwa wanandoa wengi katika jamii zetu.

Kisheria endapo umiliki huu binafsi ukiwa haujabainishwa tafsiri yake ni kuwepo na dhana ya kuwa wanandoa wote wanamiliki ardhi hiyo kwa maslahi yanayogawanyika, na msajili wa hati atatakiwa kuwaandikisha wanandoa hao wamiliki kwa pamoja kwa maslahi yanayogawanyika. Wanawake wanapaswa kutambua nafasi hii kwani ardhi au nyumba wanazoishi katika ndoa mara nyingi ni wanaume wamenunua na kuweka majina yao pekee yao, na kama haikubainishwa umiliki binafsi katika familia kwa maslahi yasiyogawanyika, ulinzi kisheria umewekwa kwa wanawake kunufaika na maslahi ya ardhi au nyumba husika kwa kuwa wengi wao huchangia nguvu kazi katika kuitunza au kuindeleza nyumba au ardhi na kuufanya ushiriki huu kumpa haki ya mgawanyo wa maslahi katika ardhi au nyumba husika

Kwa upande wa rehani ya ardhi au nyumba katika ndoa, sheria imelinda maslahi ya wanandoa wote wawili. Sheria inaelekeza pale ambapo ardhi au nyumba ya ndoa inawekwa rehani ni sharti ridhaa ya maandishi na sahihi ya mwanandoa halali wa mkopaji wanaoishi katika nyumba hiyo au kuitumia ardhi husika ipatikane na kinyume na hapo ni batili na pingamizi linaweza kufunguliwa mamlaka husika au mahakamani. Pia sheria imeainisha zaidi ni wajibu wa Mkopeshaji kabla ya kutoa mkopo kuchukua hatua za makusudi za kuthibitisha kwamba mkopaji ana ndoa na kwamba anayetoa ridhaa ni mwanandoa halali wa mkopaji. Vilevile, iwapo mwanandoa atataka kuuza, kukodisha, au kuhamisha maslahi ya hakimiliki ya ardhi au nyumba ya ndoa kwa mtu mwingine, yule atakayehamishiwa, kuuziwa, kukodishwa au kupewa ana wajibu wa kuhakikisha kama ridhaa yawanandoa wengine kama wapo imetolewa.

Kumeendelea kuweko na changamoto ya kutowashirikisha wanawake katika suala hili la rehani ya ardhi au nyumba ya ndoa hasa katika maeneo ya vijijini ambapo taasisi imekuwa ikitekeleza programu zake za utaoji wa mafunzo ya haki za ardhi, mijadala ya wazi na usaidizi wa kisheria. Hata hivyo ieleweke kwamba rehani ya kimila itafuata taratibu za kimila zinazotumika katika eneo husika. Hata hivyo kama kuna tatizo lolote juu ya rehani wahusika watatakiwa kutumia huduma ya Baraza la Ardhi la Kijiji. Pamoja na mambo mengine, Baraza la Ardhi la Kijiji litatakiwa kuangalia kama rehani ilikuwa na masharti yanayozingatia haki na taratibu za rehani ya kimila katika eneo husika. Ili taratibu zifanyike za kubatilisha rehani hiyo mwanandoa husika pia anaweza kwenda katika vyombo vya mahakama kuomba na kuweka pingamizi la rehani ili rehani hiyo ibatilishwe. Huu pia ni utaratibu kwa rehani za ardhi au nyumba zilipo mijini

Pamoja na sheria hizi, bado kuna wanawake wengi hususan vijijini na maeneo ya pembezoni mwa miji wanaoshindwa kupata haki yao ya kumiliki ardhi kutokana na kukosa kuelewa sheria hizi au jinsi ya kudai haki zao kwa mujibu wa ulinzi uliowekwa kwao katika sheria za ardhi na nyinginezo . Mila na desturi kandamizi bado zipo hivyo elimu inahitajika zaidi ili watu waachane na mila hizo na kuhakikisha wanawake wanapata haki zao kama wanavyostahili.

» Inatoka uk. 1

ikifanya kazi. Kati ya mwaka 2013 na 2015, msaada wa kisheria ulitolewa kwa wanawake wapatao 299 kati ya idadi ya watu 927 waliohudumiwa kwa kipindi hicho. Idadi hii inahusishwa wananchi waliofikiwa

katika maeneo ya programu vijijini pamoja na wananchi waliofika katika ofisi za taasisi. Kumekuwa pia na ushauri wa kisheria kwa makundi hususan kamati za wananchi zikiwemo kamati ya wananchi ya mradi wa mji mpya wa Kigamboni, Kamati ya Wananchi wa Kwembe, kamati ya wananchi wa kitongoji cha Uvinje Saadani na Kamati ya wananchi wa mradi wa upanuzi wa barabara ya Kimara Dar es Salaam.

Ni muhimu kutambua kuwa Taasisi imekuwa na utaratibu wa kutoa msaada na ushauri wa kisheria bure kwa wananchi kutokana na ukweli kuwa wananchi wengi hususan wale wanaoishi vijijini wanapata ugumu katika kuzifikia huduma hizo mijini ambako ziko kwa wingi kutokana na umbali na gharama ya nauli na tozo kutoka kwa mawakili.

Aidha, ni muhimu kutambua kuwa, msaada na ushauri wa kisheria kwa wananchi umekuwa ukitolewa pia na wangalizi wa masuala ya ardhi walioko katika kila kijiji ambacho taasisi imetekeleza programu za mafunzo. Waangalizi hawa wamepewa mafumzo maalumu ya kuwajengea uwezo ili waweze kusikiliza matatizo ya ardhi kwa wananchi na kuwashauri kulingana na mahitaji yao. Waangalizi hutuma taarifa ofisi za taasisi kila baada ya miezi mitatu ambazo kwa wastani zinaonyesha kuwa wanawake wanaopokea msaada wa kisheria kwa mwaka kwa njia hii wanakadiriwa kufikia 1,000. Maeneo ambayo waangalizi hawa

> Ni muhimu kutambua kuwa Taasisi imekuwa na utaratibu wa kutoa msaada na ushauri wa kisheria bure

# MSAADA WA KISHERIA UNAIMARISHA ULINZI WA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE.



*Wanawake kama sehemu ya jamii wamekuwa wakishiriki katika mafunzo yanayoandaliwa na HAKIARDHI kuhusiana na haki za ardhi*

wamefanya kazi kwa ufanisi ni pamoja na wilaya za Kilolo, Mufindi, Kilombero, Ulanga, Mkinga, Kilindi na Korogwe. Wilaya nyingine zenye waangalizi wa namna hiyo ni Kisarawe, Rufiji, Liwale na Morogoro vijijini.

Mfano ni Bi Esta Iigwile anaishi Morogoro wilaya ya Kilombero alifika HAKIARDHI mnamo tarehe 6/1/2014 na kupatiwa msaada wa kisheria ambao ulimjengea ujasiri wa kumkabili shemeji yake bila kumvunjia heshima na kumuomba ampatie eneo lake ambalo ni sehemu ya ardhi waliyopata kwa pamoja na marehemu mume wake. Baada ya kufanikiwa, Bi. Esta anasimulia kuwa halikuwa jambo rahisi kwake kwani alikuwa anafanya jambo lisilozoeleka na jamii kuwa ni kinyume na taratibu za mila na desturi yao. Hata hivyo baada ya kujua haki yake, aliamua kupambana kwa njia ya mahakama na hatimaye kufanikiwa kuipata ardhi hiyo inayofikia ekari mbili. Furaha ya Bi. Esta leo ni kubwa licha ya kuwa ni mjane kutokana na ukweli kuwa amepambania haki yake na kuipata baada ya kupatiwa ushauri wa kisheria. Kisa cha Bi Esta kinafaa kuwa chachu kwa wanawake wengine ambao wamekuwa wakinyanyasika kutokana na kunyang'anywa mali waliyochuma na wenza wao baada ya kufariki. Kwa mtazamo wa haraka haraka, Wanawake wanaoishi vijijini ndio nguzo ya maendeleo ya taifa kutokana na uzalishaji wanaofanya hivyo msaada wa kisheria unawawezesha kupiga hatua moja ya maendeleo na kupunguza umaskini na utegemezi. Kwa wilaya ambazo msaada wa kisheria umetolewa, kasi ya uuzaji wa ardhi holela uliokuwa ukifanywa na wanaume imepungua na hivyo kuwahakikishia wanawake kuendelea kuzalisha katika ardhi wanayotumia. Katika kijiji cha Idete Wilaya ya Kilolo, mwangalizi Loina Kikoti anakiri kuwa wanawake wa Idete wamepongeza msaada wa kisheria uliotolewa na HAKIARDHI kutokana na ukweli kuwa kasi ya uuzaji holela wa ardhi imepungua kuwasaidia wanawake walio kwenye ndoa wasiuzwe kama bidhaa wakiwa ndani ya nyumba zao.

# MILA POTOFU ZINA ATHIRI UMILIKI WA ARDHI KWA WANAWAKE

*Na. Gloria Msaki*

Kutokana na tatizo kubwa la ukandamizaji wa wanawake unaosababishwa na mfumo dume na mila potofu zinazowabagua wanawake kumiliki mali katika jamii, wanawake wengi wameendelea kukosa haki zao za msingi hasa katika kupata, kumiliki na kutumia rasilimali mbalimbali ikiwemo ardhi. Jamii imekuwa ikiwabagua wanawake na kuwaona kama hawastahili kumilikishwa ardhi kwa kutumia taratibu za kimila zinazopingana na sheria za nchi zikiwemo sheria za ardhi.

Jamii nyingi zimekuwa na mtazamo kuwa mwanamke au mtoto wa kike hastahili kurithi mali kutoka katika familia ya wazazi wake maana ni mtu wa kuolewa tu na akirithishwa mali maana yake ni kuinufaisha familia nyingine ambako ataenda kuolewa. Wengine walienda mbali zaidi kwa kuruhusu mila ya ndugu wa marehemu kurithi mjane ili kuhakikisha mali inabaki ndani ya ukoo ule ule.



*Mmoja wa wanawake aliyeshiriki mafunzo ya haki za ardhi na utawala katika kijiji cha Kidabaga wilayani Kilolo akitoa hoja yake*

Iko mifano hai kwa makabila mengi ya kanda ya Ziwa wakiwemo Wakurya, wasukuma pamoja na nyanda za juu kusini kama wahehe na wanyakyusa. Imekuwa ni jambo la kawaida sana kuona au kusikia mjane akidhulumiwa mali na ndugu wa marehemu mumewe hasa kaka au wadogo zake marehemu hadi inafikia hatua mjane anakosa haki ya kutumia mali alizochuma na marehemu mumewe na kama walibahatika kupata watoto basi familia ile inaweza kuishi maisha ya dhiki sana huku ndugu wa mumewe wakifurahia na kunufaika na mali za familia ile. Yote haya ni matokeo ya mila potofu na kandamizi dhidi ya mwanamke pale ambapo jamii inashindwa kutambua thamani ya mwanamke na haki yake katika kupata, kumiliki na kutumia rasilimali ikiwemo ardhi.

Kukua kwa jamii zetu kumeambatana na kupanuka kwa mahusiano ya watu katika jamii. Hali hii imesababisha kuwe na sheria kama taratibu za kijamii zilizo juu ya mila za makabila husika ili kuongoza na kuboresha mahusiano haya ya kijamii. mabadiliko haya yamefungua fursa kwa wanawake kupata nafasi ya kushiriki katika vyombo vya maamuzi ambamo wana nafasi sawa ya kudai, kutetea na kulinda haki zao za kumiliki mali kama ilivyo kwa wanaume.

Ili kuchochea mabadiliko na marekebisho ya sheria na hatimaye kutokomeza mila potofu, kuna haja ya serikali, mashirika yasiyo ya serikali na wale wote wanaojihusisha na kutetea haki za wanawake kujenga nguvu ya pamoja na kutoa mbinu za kufanikisha azma hiyo.

Katika dunia ya sasa ya utandawazi mila potofu zinazombagua mwanamke hazina nafasi tena ya kuachiwa zifanye kazi hasa ikizingatiwa kuwa wanawake wana nafasi katika familia na jamii kwa ujumla kuchangia pato la familia na jamii kwa kiwango kile kile wanachochangia wanaume. Swali la kujiuliza ni kuwa, je wakibaguliwa katika umiliki wa ardhi ambayo ndiyo nyenzo kuu ya uzalishaji mali, watawezaje kuchangia katika upatikanaji wa pato hilo?

Hivyo basi kuna haja ya kutoa elimu vijijini juu ya haki ya msingi kwa mwanamke maana huko ndiko wanawake wananyanyaswa juu ya haki yao ya kikatiba ya kumiliki mali kama ibara ya 24 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inavyosema "kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na haki ya hifadhi kwa mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria'.

# HATIMILIKI YA KIMILA NA ULINZI WA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE

*Na Joseph Chiombola*



*Wanawake wakipitia cheti cha hatimiliki ya kimila baada ya kukabidhiwa*

Kwa kipindi kirefu sasa wananchi kwenye makabila mengi nchini hasa waishio vijijini wamekuwa wakiishi kwa kufuata mila and desturi za makabila husika katika maisha yao ya kila siku. Mila na desturi hizo ndio huipambanua jamii au kabila fulani na kuweza kuwatofautisha na makabila mengine. Vile vile mila hizo ndizo zimekuwa zikitumika kama miongozo ya maisha yao na kuweza kufanikisha masuala mbalimbali ikiwemo sherehe, misiba na kuweza kuhamasisha shughuli za maendeleo kwenye jamii husika. Lakini pia ni lazima tukiri ya kuwa zipo mila na desturi ambazo tafsiri yake imekuwa ikitumika kuwagandamiza na kuwanyima haki za msingi baadhi ya makundi ya watu kwenye jamii au kabila fulani. Mfano wa mila hizo kandamizi ni pamoja na kutomilikishwa ardhi kwa wanawake.

Taratibu zinazohusu masuala ya umiliki wa ardhi nchini zinasimamiwa kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Ardhi 1995, Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999, Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 pamoja na sheria nyingine zinazohusiana na hizo. Sera na Sheria hizi zilikuja miaka ya 90 na kuanza kufanya kazi mwaka 2001 ambapo pamoja na mambo mengine, zinatambua matumizi ya mila katika usimamizi na umiliki wa ardhi nchini. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Kijiji namba 5 ya mwaka 1999, ardhi iliyopo ndani ya kijiji itamilikiwa kwa taratibu za kimila kwa kutolewa cheti cha hakimiliki ya kimila au bila cheti.

Hata hivyo sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999 imeweka angalizo juu ya matumizi hayo ya mila kwa kuainisha kuwa matumizi ya mila zozote ambayo tafsiri yake inamnyima haki mwanamke basi mila hiyo inapaswa kuachwa kwenye usimamizi na utoaji wa haki katika masuala la ardhi.

Wanawake hasa waishio vijijini wamekuwa kwenye hatari zaidi ya kutomilikishwa ardhi zao kutokana na uwepo wa mila kandamizi hivyo kuishia kupewa haki ya kutumia tu na si kumiliki kama wanavyomiliki wanaume. Utaratibu huu wa umiliki wa ardhi kijijini kimila umerasimishwa kwa kuandaliwa Cheti cha Hatimiliki ya Kimila ambacho hutolewa na Halmashauri ya Kijiji kwa mmiliki wa ardhi ndani ya kijiji. Cheti hiki huweza kumilikishwa kwa mtu mmoja, ama mume na mke kwa pamoja, au kikundi cha watu chenye matumizi ya pamoja ya ardhi hiyo. Vile vile kifungu cha 3(2) cha Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 vimeanisha kuwa kila mtu (Mwanaume au Mwanamke) ana haki sawa katika kupata, kumiliki, kutumia, kudhibiti na kuuza ardhi. Utaratibu huu wa kumiliki ardhi ndani ya kijiji kwa kupitia Cheti cha Hakimiliki ya Kimila ni fursa na ukombozi wa kisheria ambao kama ukitumika ipasavyo utawaondoa wanawake katika manyanyaso waliyokuwa wakiyapata katika kupata haki zao za ardhi hususani kwenye urithi, namna ya kupata, kumiliki, kuuza au kugawa ardhi sawa na haki waliyonayo wanaume.

Katika maeneo ambayo vyeti hivi vimeanza kutolewa kwa mfano katika vijiji vya Wilaya ya Kilolo ambapo HAKIARDHI kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya imewezesha mchakato wa mpango wa matumizi ya ardhi ya vijiji na upimaji wa mashamba kumekuwepo na mifano hai ya mafanikio ya wananawake kupata haki zao za ardhi kutokana na kuwa na vyeti vya hatimiliki ya kimila. Baadhi ya mifano ya wanawake hao ni kama ifuatavyo;

Katika Kijiji cha Kitelewasi Bi. Sptelazia Gwejime alipimiwa shamba na kupewa cheti cha hatimiliki ya kimila kwa jina lake, kisha shemeji yake kwa jina la Bw.Kiliyakusu Mbugi akataka kumnyang'anya shamba lake. Mgogoro huo ulifikishwa katika baraza la kata ya Ilole na baada ya usikilizwaji wa kesi yao mama Sptelazia Gwejime alipewa ushindi kwa kuwa eneo lake lilipimwa na kupatiwa hati miliki ya kimila ambapo shemeji yake alikosa uthibitisho wa kuwa ndio miliki halali wa hilo eneo.

Kesi nyingine iliyoweza kuthibitisha hatimiliki ya kimila kuwa ulinzi wa haki za ardhi kwa wanawake ni kesi ya Bi. Agnes Kabogo alishitakiwa na shemeji yake Bw.Kiliyakusi Mbugi ambapo kuna eneo la kinyungu (shamba) ambalo Bi.Agnes Kabogo alikuwa anamiliki na marehemu mume wake. Mara baada ya kufariki mume wake Bw.Mbugi alimtaka Bi Kabogo atoke katika eneo hilo. Kwa taratibu za mila ya kihehe, unapofiwa na mume wako ukoo wake unachukua maeneo. Mgogoro huu ukafikishwa katika baraza la kata ya Ilole ambapo baraza lilitoa maamuzi na kumpatia haki Bi Agnes Kabogo kwa kuwa alikuwa amelikatia hati miliki shamba hilo kwa jina lake. Wakati shemeji yake akikosa uthibitisho wa umiliki wa eneo hilo kama ni eneo la ukoo.

# Q Wananchi wanasemaje ?

## JUU YA SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI



***Elimu kwa wanawake itasaidia kutokomeza mfumo dume katika jamii. Flora Chalamila- Igombavanu Mufindi***

Mfumo dume, mila na desturi na sheria kandamizi dhidi ya mwanamke zimepitwa na wakati. Hizi ni zama za haki sawa kwa wote, hivyo tupambane kuondokana na mila potofu na kulinda haki za mwanamke. Litakuwa ni jambo la kusikitisha endapo jamii itatumia mfumo dume, ubaguzi, unyanyasaji na ukatili kumnyima mwanamke haki yake ya kumiliki ardhi. Mimi kama mwangalizi nahamasisha jamii kwa njia ya elimu kwenye mikutano ili kuwezesha wanawake kutambua haki zake na kuzidai.




***Sheria za kidini na za kimila ziangaliwe upya ili kuboresha haki ya kumiliki mali kwa wanawake-Dinani Nyomolelo, Iramba Mufindi***

Wanawake wengi wanakutana na matatizo ya mirathi hususan kwa sheria ya kiislam ambayo kwa Waislam inataka mjane kupata kiasi kidogo tu cha urithi wa mali za marehemu na sheria ya kimila ambayo inasema mjane hawezi kurithi nyumba wala ardhi ya marehemu ambayo imeendelezwa hivyo hizi ndio sababu kuu zinazosababisha wanawake kunyimwa haki yao ya kumiliki ardhi wakati waume zao wanapofariki dunia. Elimu ya masuala ya ardhi itawakomboa wanawake dhidi ya unyanyasaji huu hasa kwa wanawake wa vijijini.



***Upimaji wa mashamba na utoaji hatimiliki za kimila unasaidia kulinda haki za wanawake katika ardhi. Tuhuvilage Msigala- Kidabaga Kilolo***

Sasa ni takribani mwaka mmoja umepita tangu wanawake wa kijiji chetu waone nuru. Wao si wafanyakazi wa shambani tu bali pia wanamiliki ardhi. Upimaji wa mashamba katika kijiji hiki umewawezesha wanawake wengi kumiliki maeneo kwa hati milki ya kimila hivyo kuhamasisha wanawake wengine wapigania haki yao ya kumilikishwa ardhi katika maeneo ya familia au urithi ili waweza kuandaliwa hatimiliki za kimila ambazo tayari zimeshaonyesha kuwa ni ulinzi tosha kwa wanawake.



***Mgawanyo wa mirathi ya ardhi na mali uzingatie haki sawa kati ya wanaume na wanawake. Haji Kivelege –Idete Kilolo***

Sheria za Ardhi za mwaka 1999 tulizojifunza zimeeleza kinagaubaga kwamba mwanamke ana haki ya kumiliki ardhi pasipo kubaguliwa wala kunyanyaswa. Mimi kama mwangalizi, nimekuwa nikisisitiza haki hizo kila ninapokuwa na mikutano na vijana wenzangu ili wazingatie na kusheshimu haki za wanawake katika ardhi. Cha msingi, tuzidishe kuhamasisha wanawake wajue, wafuatilie na kudai haki zao za kumiliki ardhi. Mimi kama kijana napendelea kuona haki inatendeka ndio maana najitolea kutoa ushauri kwa masuala ninayojua kwa wanaume na wanawake hasa wajane ili wasidhulumiwe mirathi katika ugawanyaji wa mali (ardhi) waume zao wanapofariki.




***Elimu juu ya haki za ardhi iwe sehemu ya mitaala ya shule za msingi na sekondari ili kuwajengea uwezo wanawake kudai haki zao. Deus Mileta- Ihowanza Mufindi***

Wanawake wamekuwa wakisaulika katika kufanya maamuzi kuanzia ngazi ya familia mpaka serikali ya kijiji kwasababu ya mazoea ya mila na desturi potofu. Elimu ya masuala ya haki za binadamu itasaidia kuondokana na mfumo huu unaokwamisha maendeleo ya mtu binafsi na kijiji chetu pia kwa kuwabagua wanawake. Kuna haja ya kuwawezesha wasichana wakiwa mashuleni washiriki katika shughuli mbali mbali za maendeleo mapema ili wasije wakaendelea kubaguliwa wakiwa watu wazima katika vijiji vyetu.



***Wasichana wajitokeze kwenye mijadala na mikutano ili kuimarisha uwezo wao wa kufanya maamuzi kuanzia ngazi ya familia. Felista Maliga – Idasi Kilolo***

Umiliki wa ardhi kwa wasichana bado ni changamoto kubwa hapa kijijini kutokana na wazee kutumia mila na desturi mbaya ambazo hazimpi fursa mwanamke kusikilizwa. Mimi kama mwangalizi wa ardhi nimekuwa nikiomba kushiriki mijadala ya vitongoji ili kuelimisha nafasi ya msichana katika umilikaji wa ardhi. Ushauri wangu kwa wasichana kijijini ni watambue haki zao ili kuweza kuondokana na janga la unyanyasaji pindi watakapo kuwa kwenye maisha ya ndoa.




*Wanawake wakishiriki katika harakati za kutetea haki za ardhi kwenye maeneo yao kutokana na kukithiri kwa migogoro ya ardhi*

# ATHARI ZA MIGOGORO YA ARDHI KWA WANAWAKE

*Na.Cathbert Tomitho*

Migogoro ya ardhi hutokana na mgongano wa maslahi katika matumizi ya ardhi na rasilimali zilizoko kwenye ardhi baina ya watumiaji wa ardhi ambao wanaweza kuwa ni mtu mmoja, kikundi cha watu au jamii au taasisi za umma na binafsi. Kuna aina mbalimbali ya migogoro ya ardhi ikiwa ni pamoja na migogoro baina ya wakulima dhidi ya wafugaji, wanavijiji dhidi ya wawekezaji, mamlaka za hifadhi dhidi ya wanavijiji, kijiji dhidi ya kijiji, na wachimbaji wadogowadogo wa madini dhidi ya wachimbaji wakubwa.


Migogoro ya ardhi imekuwa na visababishi vingi ikiwa ni pamoja mapungufu katika mfumo wa kisheria ambao unalimbikiza mamlaka kubwa kwenye dola na watendaji wake ambao huishia kutoa maamuzi yasiyokuwa sahihi na kusababisha migogoro baina ya watumiaji wa ardhi. Sababu nyingine ni wananchi kutoshirikishwa ipasavyo katika utungaji wa sera na sheria zinazosimamia rasilimali, jamii kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusiana na sera na sheria zinazohusika na utawala wa ardhi pamoja na utatuzi wa migogoro ya ardhi, pamoja na mitazamo mibaya juu ya baadhi ya mifumo ya uzalishaji mali kama vile ufugaji na ukulima hali ambayo huchochea chuki na uhasama baina ya makundi yanayotegemea rasilimali ardhi kwa pamoja.

Migogoro ya ardhi ina athari mbalimbali kwenye maisha ya mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla. Athari hizi ni pamoja na vifo vya binadamu vinavyotokana na mapigano, uharibifu wa mali na rasilimali kama vile mifugo, nyumba, mazao na miundombinu mbalimbali. Halikadhalika, migogoro hii imekuwa na madhara katika uzalishaji wa chakula kwa jamii hasa kutokana na wasiwasi unaotanda katika maeneo migogoro na kusababisha uzalishaji kupungua au kukwama kabisa.

Wanawake ni kundi kubwa katika jamii linaloathirika na migogoro ya ardhi inayotokea maeneo mbalimbali nchini. Ni dhahiri kuwa wanawake ndio wazalishaji wakubwa katika ngazi ya familia kwenye jamii nyingi za kitanzania. Asilimia takribani 74 ya watanzania wote inapatikana kijijini wengi wao wakiwa ni wanawake ambao kazi zao za msingi ni uzalishaji mali na chakula kupitia kilimo na ufugaji. Kwa maana hiyo, migogoro ya ardhi inapoibuka, mfumo mzima wa uzalishaji mali uharibika na kuziacha familia nyingi zikiishi katika lindi la umasikini na uhaba wa chakula.

Uhaba wa chakula ni tatizo linalowakabili sana wanawake wanaoishi katika maeneo yanayokumbwa na migogoro ya ardhi mara kwa mara kutokana na wanaume kukimbia makazi yao wakihofia kukamatwa na vyombo vya dola kwa tuhuma za kuhusika kwenye migogoro ya ardhi. Halikadhalika, wanawake wamejikuta katika mzigo mzito wa kuhakikisha familia inatimiziwa mahitaji mengine ikiwa ni pamoja na mavazi na malazi. Vilevile watoto wengi hasa wa kike wamekuwa wakikosa fursa za kielimu kutokana na migogoro hasa ya wakulima na wafugaji mifano hai ikiwa katika wilaya za Kiteo, Kilosa na Mvomero kutokana na kutokuwa salama kwa wanafunzi kwenda mashuleni.

Kiuchumi, migogoro ya ardhi imewaweka pabaya wanawake kutokana na kushindwa kujihusisha na shughuli za uzalishaji mali katika kilimo na biashara. Wanawake wamejikuta wakikaa na



*Migogoro ya ardhi inapotokea uathiri shughuli za kiuchumi kama kilimo ambazo wanawake wengi ndio wazalishaji wakuu*



kujificha nyumbani kuwalinda watoto na kujilinda wenyewe kutokana na vitisho wanavyovipata kutoka kwa jamii yenye uhasama nayo katika mgogoro husika. Kwa mfano katika wilaya ya Kilosa wanawake wa jamii za wafugaji na wakulima wamekuwa wakishindwa kuzalisha mali kutokana na hofu ya kuvamiwa na kudhuriwa miili yao na mali zao.

Migogoro ya ardhi inapotokea uathiri shughuli za kiuchumi kama kilimo ambazo wanawake wengi ndio wazalishaji wakuu
Kisaikolojia, migogoro ya ardhi imekuwa ikiwaathiri wanawake wengi kutokana na kuondokewa na ndugu zao wa karibu hasa waume na watoto wao. Mfano katika kijiji cha Kiwale, Tarafa ya Malinyi wilayani Ulanga, mnamo mwaka 2012 jumla ya watu 6 waliuawa katika mgogoro baina ya wanavijiji na mamlaka za hifadhi. Mfano mwingine ni katika wilaya ya Morogoro kwenye bonde la Mto Mgongola ambapo mapigano baina ya wakulima na wafugaji katika vijiji vya Kambala, Dihombo na Mkindo hapo Novemba 2013 yalisababisha vifo vya watu 7 na majeruhi zaidi ya 36. Wanawake katika familia hizi waliachwa wapweke kutokana na kuondokewa na watu ambao ndio waliokuwa mihimili kwenye familia husika.

Migogoro inayowahusisha wawekezaji na wananchi nayo imekuwa na athari kubwa kwa wanawake. Kwa mfano katika wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya katika shamba lenye ukubwa wa hekta 1,870 ambalo awali lilimilikiwa na NAFCO na baadae mwaka 2006 kugawiwa kwa wawekezaji, ubinafsishaji wa shamba hili umeibua mgogoro mkubwa baina ya wananchi na wawekezaji kutokana na jamii kukosa maeneo ya kilimo. Waathirika wakubwa katika mgogoro huu ni wanawake kwasababu wamekuwa wakihangaika sana katika kutafuta chakula cha kulisha familia. Kadhalika wanawake katika eneo hili wamekuwa wakikumbana na uhaba wa maji kutokana na mwekezaji kuziba njia zilizotumika kupata maji.
Mfano mwingine ni mgogoro baina ya mwekezaji na wanavijiji katika wilaya ya Morogoro ambapo mwaka 2014 mwekezaji katika kijiji cha Kikundi, kata ya Makuyuni alituhumiwa kuwafanyia uharibifu wa kuwavunjia wanavijiji wapatao 50 nyumba na mali nyingine ambapo wanawake waliathirika zaidi kutokana na kutangatanga wakitafuta malazi na chakula kwa watoto.
Mifano hii michache inadhihirisha ni kwa kiasi gani tatizo la migogoro ya ardhi na athari zake kwa wanawake lilivyo kubwa. Mifano hii ichukuliwe kama somo ambalo linawakumbusha watendaji wa serikali kutimiza wajibu wake katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo utatuzi madhubuti wa migogoro ya ardhi ili kuwaepusha wanawake na jamii nzima na manyanyaso yanayotokana na migogoro ya ardhi.

Baadhi ya hatua za ukomeshaji wa migogoro ya ardhi ni pamoja na serikali kutekeleza mpango wa matumizi ya ardhi vijijini. Katika ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji wakubwa, serikali ihakikishe kuwa maslahi ya wananchi yanapewa kipaumbele. Vilevile ni muhimu serikali kuhakikisha kuwa mabaraza ya utatuzi wa migogoro ya ardhi yanaundwa kwa mujibu wa sheria na kutekeleza kazi zake kwa haki pasipo upendeleo kwa kundi lolote.



# NAFASI YA WANAWAKE KATIKA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI

*Na: Beatha Fabian*

Sheria ya Ardhi namba 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 za mwaka 1999 zimetungwa kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995. Sheria hizi zinaainisha vyombo vyenye dhamana ya kushughulikia migogoro ya ardhi na nyumba ambavyo vimegawanyika katika mifumo miwili ambayo ni mfumo wa kiutawala na wa kimahakama.

Katika ngazi ya kijiji chombo cha kiutawala ni kamati ya uamuzi wa kijiji. Na kwa upande wa kimahakama ni Baraza la Ardhi la kijiji. Upande huu unaendelea katika ngazi ya Baraza la kata, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Mfumo huu wa utatuzi wa migogoro unaoanzia katika ngazi ya Kijiji umefafanuliwa kwa kina katika sheria ya Mabaraza na Mahakama za utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Namba.2 ya mwaka 2002 ambayo imeanza kutumika tarehe 1/10/2003.

Sheria Na. 2 imefuta mamlaka ya Mahakama ya Mwanzo, Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi kusikiliza na kuamua masuala yote ya madai kuhusu ardhi. Inafuta Mabaraza ya Nyumba ya Mikoa, Baraza la Rufaa la Nyumba, Mabaraza ya Usuluhishi wa Ardhi ya Wilaya/Mikoa na Baraza la Rufaa la Ardhi. Inaunda na inatoa majukumu na mamlaka ya Mahakama zilizotajwa katika Sheria Namba.4 na 5 za mwaka 1999 kushughulikia migogoro ya ardhi na nyumba.

Nafasi ya wanawake katika mfumo huu wa kutatua migogoro ya ardhi imeainishwa kuanzia uundwaji wa vyombo vyenyewe. Kwa mfano, kamati ya uamuzi wa kijiji inaundwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji chini ya kifungu cha 53 cha sheria ya ardhi ya vijiji namba 5 ya 1999, kwa ajili ya kusuluhisha migogoro inayohusiana na mipaka ya ardhi, haki ya njia na maslahi ya wanawake, walemavu, na watu wasiokuwepo kijijini.

Kamati hii inaundwa na wajumbe wasiozidi tisa (9), ambapo wajumbe wasiopungua wanne (4) ni wanawake. Wajumbe wa kamati hii wanatumikia kwa kipindi cha miaka mitatu (3) na wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu (3). Kikao halali cha Kamati ya Uamuzi ya Kijiji kinatakiwa

kuwa na wajumbe wasiopungua watano (5), ambao wawili (2) kati yao ni lazima wawe wanawake. Mtu yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi wa Kamati ya Uamuzi ya Kijiji anaweza kukata rufani dhidi ya uamuzi huo kwenye Baraza la Ardhi la Kijiji ndani ya kipindi cha siku thelathini (30) baada ya kutolewa kwa uamuzi. Ili kamati hii iweze kuendelea na mkutano wowote utakaoitishwa ni lazima wajumbe watano wawe wamehudhuria na kati yao wawemo wajumbe wanawake wasiopungua wawili (2).

Kwa upande wa mfumo wa mahakama, ngazi ya awali kabisa ni Baraza la Ardhi la Kijiji ambalo kazi yake kuu ni kusuluhisha na kutatua migogoro yote ya ardhi kijijini. Baraza la Ardhi la Kijiji linatakiwa kuwa na wajumbe saba (7) ambapo kati yao wanawake wasipungue watatu (3). Wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kijiji wanateuliwa na Halmashauri ya Kijiji na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Kikao halali cha Baraza la Ardhi la Kijiji kinatakiwa kiwe na wajumbe wanne (4) ambapo wawili (2) kati yao ni lazima wawe wanawake.

Chombo kinachofuatia endapo mtu hajaridhika na uamuzi wa Baraza la Ardhi la Kijiji ni Baraza la Kata linaloundwa na wajumbe nane (8) kati yao wanawake wasipungue watatu (3). Wajumbe hawa wanateuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kama ilivyofafanuliwa na Sheria ya Mabaraza ya Kata ya mwaka 1985. Kwa upande wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya huongozwa na Mwenyekiti ambaye ni mwajiriwa wa Wizara ya Ardhi kwa kuzingatia vigezo vya ajira. Vigezo hivyo ni pamoja na kuwa mhitimu wa shahada ya Sheria kutoka Chuo kinachotambulika nchini. Katika Ngazi hii kuna wasaidizi saba (7) watakaosaidiana na Mwenyekiti ambapo watatu(3) kati yao ni lazima wawe wanawake.Wanateuliwa na waziri wa ardhi kwa kushirikiana na Mkuu wa Mkoa.

Mahakama kuu na Mahakama ya Rufaa huongozwa na majaji. Kuna majaji wanawake katika vyombo hivi hivyo sheria haijabagua jinsi katika mfumo wa kutatua migogoro ya ardhi nchini.

Ifahamike kwamba sharti la idadi ya wanawake katika vyombo hivi limewekwa makusudi ili kulinda maslahi ya wanawake kwani ndio watumiaji wakuu wa ardhi. Hivyo wajumbe katika vyombo hivi wanapaswa wahakikishe kuwa hakuna ukiukwaji au upendeleo ambao utaathiri maslahi ya wanawake katika migogoro wanayowasilisha katika vyombo hivi. Wito wangu kwa Wanawake ni kuhakikisha kuwa wanajitokeza na kuzitumia nafasi hizi, kwa kushiriki na kutoa mawazo yao kwa lengo la kuboresha maslahi ya wanawake, familia zao na taifa kwa ujumla.



*Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi ya HAKIARDHI pamoja na wafanyakazi wenzangu wote napenda kuwatakia wananchi wote heri ya sikukuu ya Krismasi na Mwaka mpya wa 2016 wenye haki na mafanikio kwa raia*

*Yefred Myenzi*
*Mkurugenzi Mtendaji*

# ARDHI NI UHAI

HAKIARDHI
LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE
ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 14 AGOSTI - DESEMBA 2015




## BAADHI YA MACHAPISHO

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ardhi ni Uhai 1995 | Georgis Hadjiyavanis |
| 2. | Not yet Democracy: Reforming Land tenure in Tanzania 1998 | Issa G. Shivji |
| 3. | Haki za Wamasai waishio Ngorongoro 1999 | Issa.G Shivji/Wilbert Kapinga |
| 4. | Mwongozo wa haki za Ardhi kwa wananchi wa Tanzania 2002 | Issa G.Shivji/Deus Kibamba |
| 5. | Silencies in NGOs Discourse Occasional paper No.1 2006 | Issa G.Shivji |
| 6. | The mute Plunder "Bioreosurces and disposesion in Tanzania 2008 | Ng'wanza Kamata |
| 7. | Public Perceptions on bioresources conservation in Tanzania 2008 | HAKIARDHI |
| 8. | Accumulation by land dispossession and labor devaluation 2011 | HAKIARDHI |
| 9. | Biofuels in Tanzania 2013 | HAKIARDHI |
| 10. | Local people's perception on climate change in Tanzania 2013 | Cathbert Tomitho |
| 11. | Land grabbing in a post investment Rufiji basin 2013 | Mwami&Kamata |
| 12. | Ardhi iwe nguzo katika katiba mpya 2014 | HAKIARDHI |